الدعوة الإلكترونية

# SABEEL ACADEMY

Kwa kurahisisha elimu za kisheria

# Uislam

## HATUA KWA HATUA

## Kipindi (5)

# FUNGA

Jina la mwanafunzi ..................................................



4

# FUNGA

Allah amefaradhisha kwa Waislamu kufunga mwezi mmoja katika mwaka. Ni mwezi wa Ramadhan uliobarikiwa. Ameufanya kuwa ni nguzo ya nne katika nguzo za Uislamu na ni katika majengo yake makubwa. Allah Mtukufu amesema kuwa: «Enyi ambao mmeamini, imefaradhishwa kwenu funga kama ilivyo faradhishwa kwa waliokuwepo kabla yenu, ili mpate kuwa kumuogopa Allah». (Sura Albaqara, aya 183)

Maana ya kufunga

Utukufu wa mwezi wa Ramadhani

Hekima ya kufaradhishwa funga

Ubora wa kufunga

Vinavyo funguza

Waliosamehewa na Allah kufunga

Funga ya sunna

Eid el-Fitri

# Funga ya Ramadhani

## Maana ya kufunga

Maana ya kufunga katika Uislamu: Ni kufanya ibada kwa ajili ya Allah kwa kujizuia na kuacha kula, kunywa, kujamiiana, pamoja na vitu vyote vyenye kufunguza, kuanzia kuchomoza kwa alfajiri – ambao ni muda wa adhana ya Alfajiri- mpaka kuzama kwa jua – ambao ni muda wa adhana ya Magharibi-.



**«...Basi atakayekuwa katika mji (hayuko safarini) miongoni mwenu katika mwezi (wa Ramadhani) aufunge». Sura Albaqara, aya 185.**

## Ubora wa mwezi wa Ramadhani

Mwezi wa Ramadhan ni mwezi wa tisa katika miezi ya mwezi muandamo katika kalenda ya Kiislamu. Ni mwezi bora zaidi katika mwaka. Allah ameuhusisha peke yake kuliko miezi mingine kwa sifa nyingi bora na za kipekee, na miongoni sifa hizo bora ni hizi:

1. Kwamba Ramadhan ni mwezi ambao Allah ameuhusisha na kushuka kwa Qur'ani kitabu kitukufu na bora kuliko vitabu vyote. Allah Mtukufu amesema kuwa: «Mwezi wa Ramadhani ambao imeteremshwa humo Qur'ani ikiwa ni muongozo kwa watu, na hoja zilizo wazi za muongozo na upambanuzi. Basi atakayekuwa mjini miongoni mwenu katika mwezi huu, basi afunge». (Sura Albaqara, aya 185)

2. Mtume, swallalahu alayhi wasalam, amesema kuwa: «Utakapoingia mwezi wa Ramadhani milango ya pepo hufunguliwa, na milango ya Jahanamu hufungwa, na mashetani hufungwa minyororo». (Bukhari, Hadithi Na. 3103, Muslim, Hadithi Na. 1079). Hakika Allah ameuandaa mwezi huu kwa waja wake ili waelekee kwake kwa kufanya ibada na kuacha maovu.

3. Kwamba mwenye kufunga mchana wa Ramadhani na akasimama usiku wake (kwa kuswali), Allah humsamehe madhambi yake yaliyopita. Mtume, swallalahu alayhi wasalam, amesema kuwa: «Mwenye kufunga Ramadhani kwa kuamini na kutaraji kupata malipo ya Allah, husamehewa madhambi yake yaliyopita». (Bukhari, Hadithi Na. 1910, Muslim, Hadithi Na. 760). Pia Mtume amesema kuwa: «Mwenye kusimama (kwa kuswali) katika Ramadhani kwa kuamini na kutaraji kupata malipo ya Allah, husamehewa madhambi yake yaliyopita». (Bukhari, hadithi na. 1905, Muslim, Hadithi Na. 759).



4 Kwamba ndani ya mwezi wa Ramadhani kuna usiku wenye hadhi kubwa (Lailatul Qadri), usiku ambao ni bora sana kuliko nyakati nyingine za usiku za mwaka mzima. Allah ameeleza katika kitabu chake kwamba kufanya jambo jema ndani ya usiku huo ni bora zaidi kiliko kulifanya jema hilo siku nyingi nyingine. Allah amesema kuwa: «Lailatulqadri ni bora zaidi kuliko miezi elfu moja». (Sura Alqadri, aya 3). Mwenye kusimama katika usiku huo kwa kuamini na kutaraji kupata malipo ya Allah husamehewa madhambi yake. Huo ni usiku uliopo katika siku kumi za mwisho katika mwezi wa Ramadhani, na hakuna yeyote anayejua tarehe yake kwa uhakika.

## Ubora wa kufunga

**Kufunga kuna fadhila nyingi ambazo zimeelezwa katika sheria. Miongoni mwazo ni hizi zifuatazo:**

1 Kwamba mwenye kufunga mwezi wa Ramadhani kwa kumuamini Allah, kutii amri zake, kuamini fadhila zake zilizotajwa na sheria na kuwa na matarajio ya kupata thawabu kwa Allah, atasamehewa madhambi yake yaliyopita. Mtume, swallalahu alayhi wasalam, amesema kuwa: «Mwenye kufunga Ramadhan kwa kuamini kutaraji kupata malipo ya Allah, husamehewa madhambi yake yaliyopita». (Bukhari, Hadithi Na. 1910, Muslim, Hadithi Na. 760).

2 Pia mwenye kufunga atafurahia malipo atakayoyapata wakati wa kukutana na Mola wake kwa sababu ya funga yake. Mtume, swallalahu alayhi wasalam, amesema kuwa: «Mwenye kufunga ana furaha mbili: furaha wakati wa kufungua kwake na furaha wakati wa kukutana na Mola wake». (Bukhari, Hadithi Na. 1805, Muslim, Hadithi Na.1151)

3 Peponi kuna mlango unaoitwa Arrayaan. Haingii yeyote kupitia mlango huo isipokuwa tu wenye kufunga. Mtume, swallalahu alayhi wasalam, amesema kuwa: «Hakika, peponi kuna mlango unaoitwa Arrayyaan. Wenye kufunga wataingia kupitia mlango huo Siku ya Kiama. Haingii yeyote kupitia mlango huo ila wao tu. Patatolewa tangazo kwamba: Wako wapi wenye kufunga? Watasimama. Hataingia yeyote kupitia mlango huo isipokuwa wao tu. Wakishaingia, utafungwa na hataingia yeyote kupitia hapo». (Bukhari, hadithi Na. 1797, Muslim, Hadithi na. 1152)

4 Pia Allah ameyahusisha kwake yeye tu malipo na thawabu za mfungaji. Ikiwa malipo ya mtu yanatoka kwa Mkarimu, Mtukufu, Mtoaji sana na Rahimu sana, anatakiwa ayafurahie yale ambayo Allah amemuandalia. Mtume, swallalahu alayhi wasalam, katika Hadithi Qudsiy amesema kuwa: «Matendo yote ya mwanadamu ni yake yeye isipokuwa funga. Funga ni yangu, na mimi ndiye nitakaye itolea malipo». (Bukhari, Hadithi Na. 1805, Muslim, Hadithi Na.1151)

# Hekima ya funga

**Allah amefaradhisha kufunga Ramadhani kwa hekima nyingi na faida mbali mbali katika dini na dunia, na miongonimwazo ni hizi:**

## 1 Kuthibitisha kumtii Allah na kumuogopa.

Hiyo kutokana na kuwa funga ni ibada ambayo mja anajiweka karibu ya Allah kupitia ibada hiyo kwa kuacha anavyo vipenda, na kuyazuia mataminio yake. Anaidhibti nafsi yake kwa kumcha Allah na kumuogopa kila sehemu na kila wakati, katika siri na katika dhahiri. Kwa sababu hii, Allah Mtukufu anasema kuwa: «Enyi mlio amini, mmefaradhishiwa kufunga kama walivyofaradhishiwa waliokuwepo kabla yenu ili mpate kuwa wenye kumuogopa Allah». (Sura Albaqara, aya 183)

## 2 Mazoezi ya kuacha maasi na madhambi

Mwenye kufunga ajizuiapo kufanya mambo yaliyo halali kwa kufuata amri ya Allah atakuwa na uwezo zaidi wa kuyadhibiti mataminio yake ya kutaka kufanya maasi na madhambi, atachunga mipaka ya Allah na hatajiachia katika kufanya maovu. Mtume, swallalahu alayhi wasalam, amesema kuwa: «Mtu ambaye haachi kusema uzushi na kuufanyia kazi, basi Allah hana haja ya kuacha chakula chake na kinywaji chake». (Bukhari, Hadithi Na. 1804). Maana ni kwamba: Mtu ambaye haachi uongo na kufanya uchafu katika kauli na vitendo, huyo hajayafikia makusudio ya funga.

## 3 Kuwakumbuka wenye shida na kuwasaidia

Hiyo inatokana na kwamba katika funga kuna mazoezi ya kupambana na ukata, njaa, na kuwakumbuka maskini ambao wanapambana na hali ya kutokuwa na pato la kutosha siku zote. Kwa kufunga, mja huwakumbuka ndugu zake masikini na namna wanavyoteseka na mambo mawili machungu; njaa na kiu, na kwa sababu hiyo, atafanya juhudi ya kuwasaidia na kuwafariji.



## Vinavyo funguza

**Hayo ni mambo ambayo ni lazima kwa mfungaji kijiepusha nayo, kwakuwa yanaharibu funga, nayo ni haya yafuatayo:**

1. **Kula na kunywa. Allah Mtukufu amesema kuwa:** «Na kuleni na kunyweni mpaka ubainike kwenu weupe wa alfajiri ukitengana na weusi wa usiku. Kisha timizeni funga mpaka usiku». (Sura Albaqara, aya 187)

Mwenye kula au kunywa kwa kusahau funga yake ni sahihi, na wala hana dhambi, kama Mtume, swallalahu alayhi wasalam, alivyosema kuwa: «Mwenye kusahau hali akiwa amefunga; akala au akanywa basi atimize funga yake, kwani hakuna vingine isipokuwa kwamba Allah ndiye amemlisha na kumnywesha». (Bukhari, Hadithi Na. 1831, Muslim, Hadithi Na.1155)

2. **Vitu ambavyo viko katika maana ya kula na kunywa. Mifano yake ni hii:**

- Mchanganyiko wa vimiminwa na sindano za virutubishi zinazodungwa mwilini ili kuupa mwili chakula na madini chunvi ambayo mwili unahitaji. Vyote hivi vinasimama mahali pa kula na kunywa, na kwa hiyo, vinachukua hukumu yake.
- Kumuongezea damu mgonjwa. Damu ni chakula katika mwili, na kwa hiyo, inachukua hukumu ya kula na kunywa.
- Uvutaji tumbaku kwa aina zake zote hufunguza, kwa sababu unaingiza sumu mwilini kwa njia ya kuvuta moshi.

3. **Kujamiiana kwa kuingiza** kichwa cha dhakari kwenye utupu wa mwanamke, sawa mtu awe alitokwa na manii au hakutokwa.

4. **Mtu kujitoa manii yeye mwenyewe kwa kukumbatia au kujichua, na mfano wa hayo.**

Ama kutokwa na manii kunakotekea usingizini hakuharibu funga.

Inafaa kwa mume kumbusu mkewe na mfano wa hayo, kama anaweza kuidhibiti nafsi yake ili asije akaiharibu funga yake.

5. Kujitapisha kwa makusudi. Ama mwenye kutapika bila ya utashi wake, funga haiharibiki. Mtume, swallalahu alayhi wasalam, amesema kuwa: «Mwenye kutapika hali ya kuwa amefunga, halipi funga. Na mwenye kujitapisha, alipe». (Tirmidhi, Hadithi Na. 720. Abudaud, Hadithi Na. 2380)

6. Kutoka kwa damu ya Hedhi au Nifasi. Wakati wowote damu ya Hedhi au Nifasi ikitoka dakika za mwisho wa mchana, mwanamke atakuwa amefungua. Pia wakati wowote mwanamke kama alikuwa na Hedhi akatwaharika baada ya kuchomoza kwa alfajiri, funga yake haitasihi, na siku hiyo atakuwa hakufunga, kwa mujibu wa kauli ya Mtume, swallalahu alayhi wasalam, isemayo kwamba: «Hivi si mwanamke akipatwa na Hedhi hasali na hafungi?». (Bukhari, Hadithi Na. 1850)

Ama damu itokayo kwa mwanamke kwa sababu ya maradhi, na ambayo sio Hedhi inayojulikana katika siku maalumu katika mwezi, na wala sio damu ya Nifasi ambayo hutoka baada ya kuzaa, damu aina hii haizuii kufunga.

## Watu ambao Allah amewasamehe kufunga

Allah ameyaruhusu baadhi ya makundi ya watu kutofunga kwa kuwahurumia, kuwapa wepesi na kuwaondolea uzito. Watu hao ni hawa wafuatao:

1. **Mgonjwa ambaye anadhurika kwa kufunga.** Inafaa kwake kutofunga, na atalipa swaumu hiyo baada ya Ramadhani
2. **Mwenye kushindwa kufunga kutokana na uzee au maradhi yasiotarajiwa kupona**. Inafaa kwake kutofunga, na atoe chakula kwa kila siku kumpa masikini. Atampa kiasi cha kilo moja na nusu (11/2 ) ya chakula cha mji.
3. **Msafiri wakati wa kusafri kwake na wakati wa kukaa kwake kwa muda ugenini, kwa kipindi cha chini ya siku nne.** Inafaa kwake kutofunga, na alipe swaumu hiyo baada ya Ramadhani. Allah Mtukufu Mtukufu amesema kuwa: «Na ambaye amekuwa mgonjwa au yuko safarini, basi anaruhusiwa kutofunga na analipa siku ambazo hakufunga katika siku nyingine. Allah anakutakieni wepesi na wala hakutakieni uzito». (Sura Albaqara, aya 185)
4. **Mwenye Hedhi na mwenye Nifasi.** Ni haramu kwao kufunga na wala haisihi kwao. Ni wajibu kwao kulipa baada ya Ramadhani.(Tazama uk. 96)
5. **Mjamzito na Mwenye kunyonyesha,** pindi wakihofia kupata madhara wao wenyewe au watoto wao, hawatafunga na watalipa siku hizo ambazo hawakufunga.



**Allah amemruhusu msafiri kuacha kufunga katika mwezi wa Ramadhani, na ni wajibu wake, iwapo hatafunga, kuilipa siku hiyo ambayo hakuifunga.**

## Nini hukumu ya ambaye hakufunga mchana wa Ramadhani?

Kila ambaye hakufunga bila ya udhuru ni wajibu kwake kutubu kwa Allah, kwa sababu ya kufanya dhambi kubwa na kwa kuasi amri ya Muumba Mtukufu. Analazimika kulipa siku hiyo tu (ambayo hakufunga). Lakini mtu ambaye kafungua kwa kujamiiana, yeye atalipa siku hiyo (ambayo hakufunga) na pamoja hilo atalazimika kutoa Kafara kwa sababu ya dhambi hiyo, kwa kumuachia huru mtumwa; kumnunua mtumwa Muislamu na kumuachia huru. Uislamu unahimiza kumkomboa mwanadamu aondokane na utumwa na utwana, katika kila fursa inayojitokeza. Ikiwa hakuna mtumwa kama ilivyo hivi sasa, basi atafunga miezi miwili mfululizo. Kama hawezi kufunga, atawapa chakula masikini sitini.

## Funga za sunna

Allah amefaradhisha kufunga mwezi mmoja katika mwaka. Lakini amehimiza kufunga siku nyingine pia kwa mtu ambaye katika nafsi anaona kuwa anao uwezo na utashi wa kufanya hivyo kwa ajili ya kutaka kujiongezea malipo na thawabu. Miongoni mwa siku hizo ni hizi:



1 **Siku ya Ashura** na siku moja kabla yake au baada yake. Siku ya Ashura ni siku ya kumi katika mwezi wa Muharram, mwezi wa kwanza katika kalenda ya Kiislamu. Hii ni siku ambayo Allah alimuokoa Mtume Mussa kutoka kwa Firauni na kumuangamiza yeye na jeshi lake. Muislamu anafunga siku hii kwa ajili ya kumshukuru Allah juu ya kuokolewa kwa Mussa, na kwa ajili ya kumuiga Mtume, swallalahu alayhi wasalam, pale alipoifunga siku hii na kusema kuwa: «Fungeni siku moja kabla yake au siku moja baada yake». (Ahmad, Hadithi Na. 2154). Na Mtume, swallalahu alayhi wasalam, alipoulizwa kuhusu kufunga siku hii alijibu kwamba: «Inafuta madhambi ya mwaka uliopita». (Muslim, Hadithi Na. 1162).

2 **Siku ya Arafa.** Hii ni siku ya tisa katika mwezi wa Dhul Hijja, mwezi wa kumi na mbili katika kalenda ya Kiislamu. Mahujaji hukusanyika katika siku hii sehemu inayoitwa Arafa, wakimuomba Allah na kujipendekeza kwake. Ni siku bora zaidi katika mwaka. Inatakiwa na sheria kwa wasiokuwa katika ibada ya Hija waifunge. Mtume, swallalahu alayhi wasalam, alipoulizwa kuhusiana na kufunga siku ya Arafa alisema kuwa: «Inafuta madhambi ya mwaka uliopita na mwaka ujao». (Muslim, Hadithi Na. 1162).

3 **Siku sita za mwezi wa Shawali.** Shawali ni mwezi wa kumi katika kalenda ya Kiislamu. Mtume, swallalahu alayhi wasalam, amesema kuwa: «Mwenye kufunga Ramadhani kisha akafuatishia kufunga siku sita katika mwezi wa Shawali inakuwa kama kufunga mwaka mzima». (Muslim, Hadithi Na. 1164)

4 **Kufunga siku tatu kila mwezi.** Amenukuliwa Abuhuraira, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa: «Ameniusia kipenzi changu mambo matatu nisiyaache mpaka nife: Kufunga siku tatu kila mwezi, na swala ya Dhuhaa, na kulala baada ya kuswali swala ya Witri». (Bukhari, Hadithi Na. 1178, Muslim, Hadithi Na. 721)

# Eid (Sikukuu)

Eid ni katika matukio makubwa ya dini. Mtume, swallalahu alayhi wasalam, alipofika Madina aliwakuta Ansaar (Waislamu wa Madina) wakicheza na kushereheka siku mbili kila mwaka. Aliwauliza: «Siku mbili hizi ni za nini? Wakajibu: Tulikuwa tukisherehekea siku mbili hizi katika ujinga (kabla ya Uislamu). Mtume, swallalahu alayhi wasalam, akasema kuwa: «Hakika, Allah kwa siku mbili hizi amekubadilishieni siku mbili nyingine ambazo ni bora zaidi kuliko hizo; siku ya kuchinja na siku ya kufungua swaumu». (Abudaudi, hadithi Na. 1134). Mtume, swallalahu alayhi wasalam, akiweka wazi kwamba siku za Idi ni matukio makubwa ya dini, amesema kuwa: «Kwa hakika, kila watu wana sikukuu, na hii ni sikukuu yetu». (Bukhari, Hadithi Na. 909. Muslim, Hadithi Na. 892)



Waislamu huko India wakisali swala ya Eid.

## Eid katika Uislamu

Eid katika Uislamu ni siku ambayo furaha inaonekana wazi kwa kukamilisha ibada, ikiwa ni kumshukuru Allah kwa muongozo wake na msaada wake wa kuwezesha kufanya ibada. Sheria inataka siku hiyo watu wote kuwa na furaha kwa kuvaa nguo nzuri sana, kuwasaidia wenye shida na kufanya mambo yote ya halali kama shamrashamra na matamasha yanayoleta furaha kwa watu wote na kuwakumbusha neema za Allah kwao.

## Sikukuu za Waislamu

Waislamu wana sikukuu mbili katika mwaka wanazozisherehekea. Haifai kuainisha siku nyingine na watu wakaifanya sikukuu badala ya sikukuu hizo, na ambazo ni

**Eid-elfitri**

**ambayo ni siku ya kwanza katika mwezi wa Shawali, na**

**Eid-el-adh-haa**

**ambayo ni siku ya kumi katika mwezi wa Dhul-hijja.**

## Eid-elfitri

Ni siku ya kwanza katika mwezi wa Shawali, mwezi wa kumi. Inakuja baada ya kumalizika kwa usiku wa mwisho wa mwezi wa Ramadhani. Kwa sababu hii, imeitwa Eid-elfitri kwakuwa watu wanamuabudu Allah kwa kufungua siku hii kama walivyomuabudu kwa kufunga mwezi wa Ramadhani. Wanasherehekea Eid kwa kumshukuru Allah juu ya kukamilika kwa neema na fadhila za Allah kwa kuwarahisishia kukamilisha funga ya mwezi mtukufu wa Ramadhani. Allah mtukufu amesema kuwa: «Na ili mtimize hisabu (ya siku za Ramadhani), na ili mumtukuze Allah kwa kuwaongozeni na ili mpate kushukuru». (Sura Albaqara, aya 185)

### Nini kinatakiwa na sheria kufanywa siku ya Eid-elfitri?

1 **Swala ya Eid:** Hii ni swala ambayo Uislamu umeisisitiza sana na kuwahimiza Waislamu watoke kwenda kuisali ikiwa ni pamoja na wanawake na watoto. Wakati wake ni kuanzia kunyanyuka kwa jua kiasi cha mkuki baada ya kuchomoza mpaka jua linapokengeuka

**Namna ya kuswaliwa:** swala ya Eid ni rakaa mbili. Katika rakaa mbili hizo imamu anasoma Qur'ani kwa sauti ya juu, na atatoa hotuba mbili baada ya swala. Katika swala ya Eid inatakiwa kuzidisha Takbira mwanzo wa kila rakaa. Atatoa takbira sita mbali na Takbira ya kuanzia swala katika rakaa ya kwanza kabla ya kuanza kusoma, na katika rakaa ya pili atatoa Takbira tano mbali na Takbira ya kusimama kutoka katika kusujudu

2 **Zakatul fitri:** Allah amewajibisha kwa mtu ambaye anamiliki ziada ya chakula anachohitaji katika siku ya Eid kutoa kiasi cha pishi ya chakula kinachopendwa katika mji, kama vile mchele, ngano au tende. Atoe kuwapa Waislamu fukara na masikini, ili kusiwe na mwenye shida katika siku ya Idi.

**Wakati wa kuto Zakat fitri:** kuanzia magharibi ya siku ya Mwisho ya Ramadhan mpaka kuswaliwa Idd na inafaa kutoa kwa kutanguliza kabla ya Eid kwa siku moja au mbili.

**Kipimo chake ni pishi moja ya chakula kinacho pendwa na watu wa mji husika, kama vile mchele au ngano au tende na mfano wake. Pishi moja kwa vipimo vya kisasa ni karibu sawa na kilo tatu (3kg).**

**Ni kujitolea mwenyewe na kumtolea ambaye mahitaje yake yanamlazimu yeye, kama vile mkewe, na watoto wake. Inapendekezwa pia kumtolea zaka hii mtoto aliyeko tumboni (mimba). Atamtolea kila mmoja pishi; yaani:** Takriban kilo tatu (3kg).

Mtume, swallalahu alayhi wasalam, amefaradhisha zaka hii ili «Kumsafisha mfungaji kutokana na kauli za kipuuzi na vitendo vichafu na pia kuwapatia chakula masikini. Mwenye kuitoa kabla ya swala, inazingatiwa kuwa ni Zaka yenye kukubaliwa, na mwenye kuitoa baada ya swala, hiyo ni sadaka kama sadaka nyingine». (Abudaud, Hadithi Na.1609).

3 **Sheria inataka furaha na bashasha zionekane** katika familia; kwa watoto, wakubwa, wanaume na wanawake kwa kutumia kila jambo ambalo ni halali. Pia kuvaa nguo nzuri sana na kumuabudu Allah kwa kutofunga kula mchana wa siku hiyo. Kwa ajili hiyo, inakuwa haramu kufunga siku ya Eid.

4 **Sheria inataka kumtukuza Allah** kwa Takbira (Allahu Akbar) usiku wa siku ya Eid na wakati wa kwenda kuswali swala ya Eid. Wakati wa Takbira unamalizika kwa kuswali swala ya Eid. Kumtukuza Allah kwa Takbira (Allahu Akbar) ni kuonesha furaha kwa kumaliza funga ya mwezi mtukufu wa Ramadhani, na ni kushukuru neema ya Allah kwetu na kutuongoza tukaweza kufunga. Allah Mtukufu amesema kuwa: «Na ili mtimize hisabu (ya siku za Ramadhani), na ili mumtukuze Allah kwa kuwaongozeni na ili mpate kushukuru». (Albaqara 185) .

Namna ya kutoa Takbira: Allahu Akbar (Allah ni mkubwa sana). Allahu Akbar (Allah ni mkubwa sana). Laa ilaaha illa-llaahu Allahu Akbar (Hakuna mwenye haki ya kuabudiwa ila yeye tu. Allah ni mkubwa sana). Allahu Akbar walillaahil-hamdu (Allah ni mkubwa sana, na anazistahiki Allah tu shukurani).

Pia aseme: Allahu Akbar Kabiiraa (Allah ni mkubwa sana tena sana). Walhamdulillahi Kathiiraa (Na shukurani nyingi ni za Allah). Wasubhaanallaahi Bukratan wa-aswiilaa (Na Allah ametakasika wakati wote).

Sheria inawataka wanamume kutoa Takbira kwa sauti ya juu kwa namna ambayo haitawakera au kuwasumbua watu wengine. Wanawake wataleta Takbira kwa sauti ndogo.

## Eid-el-adh`haa (Eid-elhaj)

Hii ni sikukuu ya pili Waislamu. Sikukuu hii inakuja katika siku ya kumi katika mwezi wa Dhul Hijja (mwezi wa kumi na mbili katika kalenda ya Kiislamu). Kuna ubora mwingi, katika siku hii, mfano:

1 Siku hii ni miongoni mwa siku bora sana katika mwaka. Siku bora zaidi katika mwaka ni siku kumi za mwanzo za mwezi wa Dhul Hijja (Mfungotatu), kama Mtume, swallalahu alayhi wasalam, alivyosema kuwa: «Hakuna siku ambazo kufanya jambo jema kunapendwa sana na Allah kuliko siku kumi hizi. Swahaba waliuliza: Kuliko hata kupigana Jihadi katika njia ya Allah ewe Mtume wa Allah? Mtume alijibu: Kuliko hata kupigana Jihadi katika njia ya Allah, isipokuwa tu mtu ambaye alitoka (kwenda kwenye Jihadi) yeye mwenyewe na mali yake kisha hakurejea na chochote». (Bukhari, Hadithi Na. 926. Tirmidhiy, Hadithi Na. 757)



**Kauli ya Allah isemayo kuwa: «Basi Swali kwa ajili ya Mola wako na chinja» Sura Alkauthar, aya 2 imefasiriwa kwamba swala hapo ni swala ya Eid na kuchinja ni kuchinja mnyama wa Udh-hiya.**

2 Kwamba hii ni Siku Kubwa sana ya Hija. Katika siku hii kuna matendo makubwa sana ya Hija. Muhimu zaidi na matukufu zaidi ni kama kutufu Alkaaba, kuchinja mnyama na kuurushia vijiwe mnara wa Akaba.

### Nini kinatakiwa na sheria kufanywa katika siku ya Eid-el-adh`haa?

Katika siku ya Eid-el-adh`ha, sheria inamtaka mtu ambaye hayuko katika ibada ya Hija kufanya yale yanayotakiwa kufanywa katika Id-efitri, na maelezo yake yametangulia kuelezwa (uk 119), isipokuwa tu Zakaatulfitr. Zaka hiyo ni maalumu kwa Id-elfitri tu.

Eid-el-adh`haa ina sifa ya kipekee kwamba imependekezwa kuchinja mnyama kwa lengo la kutaka kujiweka karibu na Allah.

**Udh-hiya**: Huyu ni ngamia au ng`ombe au mbuzi au kondoo anaye chinjwa katika siku ya Eid-el-adh`haa baada ya swala Eid mpaka kuzama kwa jua siku ya kumi na tatu katika mwezi wa Dhul Hijja, kwa lengo la kutaka kujiweka karibu na Allah. Allah Mtukufu amesema kuwa: «Swali kwa ajili ya Mola wako, na chinja (kwa ajili ya Mola wako)». (Sura Alkauthar, aya 2). Neno swala katika ayah ii limetafsiriwa kwa maana ya swala ya Eid, na kuchinja kumetafsiriwa kwa maana ya kuchinja mnyama wa Udh-hiya.

**Hukumu yake:** Ni sunna iliyosisitizwa kwa mtu mwenye uwezo wa kuchinja. Muislamu atachinja Udh-hiya kujichinjia yeye mwenyewe na familia yake.

Sheria inamtaka mtu anapotaka kuchinja asiondoe (asikate) kitu chochote katika nywele zake wala kucha zake na ngozi yake, kuanzia siku ya kwanza ya mwezi wa Dhulhijja mpaka wakati wa kuchinja Udh-hiya.

## Masharti ya mnyama anaechinjwa Udh-hiya

1 Ni sharti mnyama awe katika jamii ya wanyama wafugwao ambao ni mbuzi, kondoo, ng`ombe au ngamia. Haisihi kuchinja Udh-hiya ndege au wanyama wasiokuwa hao.

Mbuzi mmoja anatosha mtu kujichinjia yeye mwenyewe na familia yake. Pia inafaa watu saba kushirikiana kuchinja ng`ombe mmoja au ngamia mmoja

2 Mnyama awe ametimiza umri unaotakiwa. Umri unaotakiwa kwa kondoo ni miezi sita, kwa mbuzi mwaka mmoja, kwa n'gombe miaka miwili na kwa ngamia miaka mitano.

3 Mnyama asiwe na dosari za wazi. Mtume, swallalahu alayhi wasalam, amesema kuwa: «Aina nne ya wanyama hawafai kuchinjwa Udh-hiya: Mwenye chongo ambaye chongo yake iko wazi, mgonjwa ambaye ugonjwa wake uko wazi, mlemavu wa mguu ambaye ulemavu wake uko wazi na aliyekonda ambaye hana mafuta». (Annasaai, Hadithi Na. 4371. Attirmidhi, Hadithi Na. 1497).

## Mnyama aliyechinjwa Udh-hiya anatakiwa kufanywa nini?

- Ni haramu kuuza chochote katika mnyama wa Udh-hiya.
- Inapendekezwa kuigawa nyama yake katika mafungu matatu. Theluthi moja atakula yeye, theluthi ya pili atatoa zawadi na theluthi iliyobaki atatoa sadaka kwa watu masikini.
- Inafaa kwa Muislamu kumuakilisha mwenzake na kutoa pesa kwa taasisi za Kiislamu zenye kuaminika ambazo zitasimamia jukumu la kuchinja Udh-hiya na kugawa kwa wenye shida.